JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZAMIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA MANYONI

Unapojibu tafadhali taja

KUMB. Na. HW/MAN/ANM/I/1 22 Februari, 2022

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA KUKUSANYA TAARIFA ZA ANWANI ZA MAKAZI NA POSTIKODI.

Mkurugenzi mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni anapenda kuwatangazia vijana wenye sifa nafasi za ajira ya muda kwa nafasi za wakusanya taarifa za anwani ya makazi kwenye kata na mitaa yote ya Halmashauri ya Manyoni.

A. SIFA ZA MUOMBAJI

i. Awe raia wa Tanzania mwenye umri kati ya miaka 18 – 35.
ii. Awe na elimu ya kidato cha nne na kuendela.
iii. Awe anajua kutumia / anamiliki simu janja yenye uwezo wa kukaa na chaji siku nzima.
iv. Awe na barua pepe na nywila inayofanya kazi.
v. Awe na uwezo wa kusoma ramani za mitaa.
vi. Awe ni mkazi wa kata husika.
vii. Malipo ya Kazi ya kukusanya taarifa za Anuani ya Makazi kwa siku ni **shilingi elfu ishirini** (**20,000/=**).
viii. Kazi ya kukusanya taarifa za Anuani ya Makazi itafanyika kwa muda wa siku saba (7)

B. KA**ZI NA MAJUKUMU**

i. Kugawa / kuandika namba za nyumba , viwanja na maeneo ya kutolea huduma.
ii. Kukusanya taarifa za nyumba, viwanja na maeneo ya kutolea huduma.
iii. Kukusanya taarifa za wamiliki wa nyumba, viwanja na maeneo ya kutolea huduma kwa kutumia mfumo wa anwani za makazi.
iv. Kutuma taarifa (data uploading) kwenye kanzidata ya mfumo wa anwani ya makazi.

C. VIAMBATANISHO VYA MAOMBI

i. Nakala ya cheti cha kuhitimu elimu ya kidato cha nne na kuendelea.

ii. Nakala ya cheti cha kuzaliwa.

iii. Picha za rangi (Passport size) 2.

iv. Barua ya maombi iliyopitishwa na Afisa Mtendaji wa Kata au Kijiji husika.

D. JINSI YA KUTUMA MAOMBI

Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono zikiwa na anwani kamili ya mwombaji na namba ya simu. Barua zote za maombi ziwasilishwe Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri kwa kutumia anwani ifuatayo;

MKURUGENZI MTENDAJI,

HALMASHAURI YA WILAYA,

S.L.P 60,

MANYONI.

E. MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI

Mwisho wa kupokea barua za maombi ya ajira za anwani ya makazi ni tarehe **26/02/2022** saa **9:30 Alasiri.**

MELKIZEDECK O. HUMBE

MKURUGENZI MTENDAJI

HALMASHAURI YA WILAYA YA MANYONI

MKURU... ...NDAJI
HAL... ...AYA
MANYONI